

# Maofisa ugani sasa kufuatiliwa kidijitali



Hawa Mathias, Mwananchi  
hmathias@mwananchi.co.tz

**'Tunataka kujenga misingi ya uadilifu, uwajibikaji na usikivu kwa wadau kwa maofisa ugani kufanya kazi kwa weledi na kuondoa vikwazo vya uwekezaji nchini ambavyo vinapunguza mapato ya Serikali.'**

**Tixon Nzunda, katibu mkuu.**

Mbeya. Katika jitihada za kudhibiti uzebe, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepanga kuwaingiza kwenye mfumo wa kielektroniki maofisa ugani wote kwa lengo la kufuatilia utendaji kazi wao.

Mpango huo umebainishwa na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tixon Nzunda kwenye kikao cha wadau kilichotoa taarifa ya utendaji wa wizara na utoaji wa vibali vya usafirishaji mifugo kielektroniki unaotarajia kuanza Julai mosi.

"Tunataka kujenga misingi ya uadilifu, uwajibikaji na usikivu kwa wadau kwa maofisa ugani kufanya kazi kwa weledi na kuondoa vikwazo vya uwekezaji nchini ambavyo vinapunguza mapato ya Serikali," alisema Nzunda.

Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Dk Daniel Mushi alisema utoaji vibali kielektroniki kutaruhisisha usafirishaji na kuwapunguzia gharama wafanyabiashara.

"Mfumo huu utakuwa mwarubaini na utaisaidia bodi kufanya kazi kwa weledi na kwa uwazi na uwajibikaji hivyo kuleta mabadiliko tasnia ya mifugo nchini," alisema.